Chanjo za COVID-19 za Vijana
Kufahamu Ridhaa

Vaccinate WA
CovidVaccineWA.org

Chanjo za COVID-19 sasa zinapatikana kwa vijana wa miaka. Watoaji wengi wanahitaji ridhaa kutoka kwa mzazi au mlezi ili kuwapa watu wa chini ya miaka 18 chanjo. Hata hivyo, iwapo una umri wa chini ya miaka 18 na una uhuru kutoka kwa wazazi wako, unaweza kujitolea ridhaa katika baadhi ya hali au kupata ridhaa kupitia shule yako iwapo huna nyumba au huna mzazi au mlezi. Waraka huu unaonyesha aina tofauti za ridhaa zinazoruhusiwa chini ya sheria ya jimbo, jinsi ya kupata mtoaji anayeweza kukuhudumia, na jinsi ya kujiandaa kwa ajili ya miadi yako ya chanjo.

Watu wazima ambao wanaweza kukutolea ridhaa:

- Mzazi
- Mlezi au mlezi chini ya sheria
- Mzazi au mtu mwingine aliyeidhinishwa na korti kutoa ridhaa kwa utunzaji wa kimatibabu kwa mtoto ndani na nje ya uwekaji wa nyumbani (Aya ya 13.32A au 13.34 Revised Code of Washington (RCW, Msimbo wa Washington Uliohakikiwa)
- Mtu ambaye amepewa uidhinishaji uliotiwa saini ili kufanya maamuzi ya utunzaji wa afya kwa ajili yako
- Jamaa anayewajibikia utunzaji wako wa afya
- Muuguzi wa shule, mshauri nasaha, au ushirikiano wa asiye na makao (iwapo umefafanuliwa kama mtu asiye na makao chini ya McKinney-Vento Homeless Education Act)*

Unaweza kujitolea ridhaa iwapo:

- **Una uhuru chini ya sheria.** Una umri wa miaka 16 au zaidi na umeomba na kupewa uhuru kutoka kwa wazazi wako.
- **Umeolewa au kuoa mtoto au mtu mzima aliyepewa uhuru.**
- **Mtoaji huamua kuwa wewe ni mtoto aliyekomaa** chini ya Mature Minor Doctrine (Kanuni ya Mtoto Aliyekomaa).**

***Maelezo zaidi kuhusu ridhaa kwa kutumia McKinney-Vento:**

Chini ya sheria ya jimbo, wauguzi wa shule, washauri wa shule, na watoaji ushirikiano wa mwanafunzi asiye na makao wameidhinishwa kutoa ridhaa ya chanjo kwa kijana au mtu mzima mdogo asie na makao (ilivyofafanuliwa chini ya McKinney-Vento homeless education act katika shirikisho - Kiingereza pekee) ambaye hayupo chini ya uzuiaji wa kimwili wa mzazi au mlezi.

Kiungo cha rasilimali: National Center for Homeless Education, *Kusaidia Elimu ya Wanafunzi Wasio na Wasimamizi ambao Hawana Makao,* https://nche.ed.gov/wp-content/uploads/2018/10/youth.pdf - Kiingereza pekee

****Taarifa zaidi kuhusu Mature Minor Doctrine**:

Baadhi ya watoaji huduma huruhusu watoto kutoa ridhaa halali chini ya "Mature Minor Doctrine" iwapo wanaweza kufahamu au kushukuru athari za utaratibu wa kimatibabu.

Katika kuamua kama mgonjwa ni mtoto aliekomaa, watoaji huduma watatathmini umri wa mtoto, werevu, ukomavu, mafunzo, uzoefu, uhuru wa kiuchumi au ukose wake, tabia ya jumla kama mtu mzima na uhuru kutoka kwa udhibiti wa wazazi wake.

Watoaji huduma hukubali ridhaa katika njia mpya tofauti.

- Ridhaa ya kinywa (kwenye simu au ana kwa ana)
- Ridhaa iliyoandikwa (fomu)
- Wengine wanahitaji ridhaa iliyoandikwa na inayosemwa.
- Ridhaa ya mtu mwenyewe kutoka kwa mtu mzima anayetoa ridhaa kwa niaba yako.

Vidokezo vya kupokea chanjo

- ☐ **Tumia chaguo za kuchuja kwenye Vaccine Locator (Kitambuaji Chanjo) (**https://vaccinelocator.doh.wa.gov/?language=sw**) au mpigie mhudumu simu ili kuona aina ya ridhaa ambayo mtoaji huduma anakubali.** Chaguo za kuchuja ambazo zinawafaa vijana kwenye Vaccine Locator zitakusaidia kupata mtoaji atakayefanya kazi na hali yako. Kwa mfano, iwapo una mtu mzima anayeweza kukutolea ridhaa lakini hawezi kwenda nawe kwenye miadi, tafuta mtoaji anayekubali ridhaa iliyoandikwa.
- ☐ **Tafuta maeneo ya chanjo yanayokubali kwenda katika kituo binafsi au kupiga simu ili kuwa na miadi,** iwapo huna mzazi/mlezi anayeweza kujaza fomu hiyo mtandaoni**.** Watoaji wengi huduma huomba kuwa mzazi au mlezi aweze kujaza fomu ya ridhaa ili kutoa miadi mtandaoni.
- ☐ **Angalia na shule yako.** Iwapo unapitia ukosefu wa nyumba, McKinney-Vento inaweza kutumika kwako. (Tazama sehemu ya mbele ili kupata maelezo zaidi.) Unaweza kufanya kazi na muuguzi wa shule, mshauri wa shule, au mwakilishi wa mwanafunzi asiye na makao kutoa ridhaa.
- ☐ **Jiandae kwa aina ya ridhaa unazohitaji kutoa:**
  - ☐ Iwapo mtu mzima anahitaji kuwepo katika miadi yako, ratibu na wao.
  - ☐ Iwapo mtoaji anakubali ridhaa iliyoandikwa, tazama iwapo mtu anayekutolea ridhaa anaweza kuchapisha na kusaini fomu hiyo.
  - ☐ Iwapo wewe ni mtoto aliepewa uhuru au mtoto aliyeolewa na mtoto aliye na uhuru au mtu mzima, unaweza kuhitaji kuleta nyaraka.
  - ☐ Iwapo unapokea ridhaa kwa kutumia McKinney-Vento, na una wasiwasi kuwa mtoaji atakuwa na maswali, unaweza kuleta nakala ya kanuni ya Ridhaa ya Kuarifiwa: RCW 7.70.065 – Kiingereza pekee na kuangazisha sehemu maalum kwa shule. (Kiungo cha kanuni: https://app.leg.wa.gov/RCW/default.aspx?cite=7.70.065 - Kiingereza pekee). Kumbuka: Hii SI mahitaji.
  - ☐ Iwapo unatafuta kutoa ridhaa kupitia kwa Kanuni ya Mtoto Aliyekomaa, huenda ukahitaji kutoa nyaraka na taarifa inaoonyesha kuwa una uhuru kutoka kwa wazazi wako. Hii haihitajiki na watoaji wote lakini inaweza kusaidia. Baadhi ya watoaji hawafanyi uamuzi wa mtoto aliyekomaa kwenye kituo lakini wanakubali uamuzi wa mtoto aliyekomaa kutoka kwa watoaji waliotangulia.

Washington State Department of Health

DOH 825-018 December 2021 Swahili
Ili kuomba waraka huu katika muundo mwingine, piga simu 1-800-525-0127. Wateja ambao ni viziwi au wasio na uwezo wa kuzungumza, tafadhali piga simu 711 (Washington Relay) au tuma barua pepe civil.rights@doh.wa.gov.